# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS-TAMISEMI

**Namba za simu** **Shule ya Secondary Mwendakulima,**
**Mkuu wa shule: 0756-521089. / 0688719713** **S.L.P 23,**
**Kahama.**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0757730908**
**0657309089.**
**Matron: +255758-968080.**
**Mhasibu: 0714944427/0756478428**

**Mzazi/ Mlezi wa ……..(**Jina la mwanafunzi**)**
**S.L.P: ……**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022 SHULE YA SEKONDARI MWENDAKULIMA ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA MKOA WA SHINYANGA.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2022 tahasusi ya …… Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe**…….** Mwisho wa kuripoti ni siku 14 baada ya tarehe ya kuripoti kama ilivyoelekezwa na **TAMISEMI**.

Shule ipo mkoani Shinyanga, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kilomita 5½ kutoka Kahama mjini na kilomita 1½ kutoka barabara kuu iendayo Shinyanga kando kando ya mgodi wa Buzwagi. Shule ipo karibu sana na shule ya sekondari ya wasichana Queen of Family.

Kwa kutokea kituo cha mabasi Kahama mjini chukua usafiri wa pikipiki au bajaji na uingilie kulia kilipo kibao cha shule sambamba na kibao cha shule ya wasichana Queen of Family. Kutoka hapo ni umbali wa kilomita 1½ tu mpaka shuleni.

Wale wanaotokea Mwanza, Shinyanga, Dar es Salaam, hawana haja ya kufika Kahama mjini,baada ya kuvuka mzani wa Buzwagi telemkia kilipo kibao cha shule sambamba na kile cha shule ya Queen of Family kutoka hapo ni kilomita 1½ kushoto kwako.

**NB: MZAZI USIFANYE MALIPO MPAKA ITAKAPOFIKA TAREHE 01/07/2022 (mwaka mpya wa fedha) Wasiliana na mhasibu kupata namba ya malipo.**

**KURIPOTI NI KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI NA MWISHO WA KURIPOTI NI SAA 11:30 JIONI.**

**2.1 Sare ya shule**

a) Sare ya shule hii ni sketi angalau mbili (02) za kijani iliyoiva (**dark green**) ndefu mpaka chini kwenye visigino vya miguu.( Mshono- Rinda box) Kwa maelezo zaidi kipande cha kitambaa cha sketi kimeambatanishwa).

b) Shati Nyeupe angalau mbili (02) mikono mirefu

c) Hijab nyeupe (juba-nyeupe) ifanane na sare ya shule.(Kwa waislamu tu)

d) Sweta moja la mikono mirefu rangi ya kijani iliyoiva (dark green-hai).

e) Tisheti moja yenye nembo ya shule- rangi ya kijivu

f) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba -Soli fupi.

g) Tai moja rangi ya kijani yenye mistari myeupe (Imeambatanishwa kwenye picha).

h)Gauni angalau mbili(**02**)za kushindia **(shamba dress)** kitambaa draft ndogo**,**angalia sampo ya kitambaa iliyoambatanishwa.

i) Soksi nyeupe jozi mbili (**02**) **ndefu. (STOCKING)**

**NB:***Kwa ufafanuzi/msaada zaidi wa uniform wasiliana na matron wa shule hasa wale wa mikoa ya mbali na shinyanga kwa namba hiyo hapo juu.Kama hujapata sampo ya kitambaa tafadhali wasiliana nasi kwa namba hapo juu.usishone kwa kukisia rangi ya kijani tu.*

**2.2 Ada na Michango ya Shule**

**a)** Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=.** Unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000/=** kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.

**b) Michango Mingine ya Shule.**

i) Tsh. **15,000/=** kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii) Tsh. **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii) Tsh. **20,000/=** kwa ajili ya taaluma.
iv) Tsh. **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v) Tsh. **2,000/=** nembo ya shule.
vi) Tsh. **10,000/=** kwa ajili ya huduma za afya/ matibabu (Yaani Tsh **5,000/=** ni kwa ajili ya huduma ya kwanza na Tsh **5,000/=** ni kwa ajili ya Bima ya Afya).
vii) Tsh. **20,000/=** ni kwa ajili ya mitihani ya kujipima (**Mock**).
viii) Tsh. **5,000/=** Fedha ya tahadhari (**Haitarejeshwa**).

Angalizo: Jumla ya michango yote ni shilingi **178,000/= (Yaani 70,000/=** kwa ajili ya ada na **108,000/=** kwa ajili ya michango mingine ya shule).

Fedha ya Ada Tsh. **70,000/=** na michango mingine (**Tsh.108,000/=)**ya hapo juu ilipwe kwenye Akaunti ya shule **A/C NO: 3061200127 NMB**- Jina MWENDANDAKULIMA CAP.

(**Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip** na sio jina la mzazi au mlezi.

**Njoo na risiti ya malipo siku ya kuripoti shuleni.**

**c) Mahitaji muhim kw Mwanafunzi**

i) Form four result slip(copy)
ii) Ream moja (**01**) ya karatasi (kwa muhula).
iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia tu.
v) Scientific calculator na madaftari makubwa (counter books) kulingana na tahasusi na kalamu za wino za kutosha.
vi) File **01**,
vii)Tochi ya solar –muhimu (umeme unapokuwa umekatika)
viii)Sanduku(loka).
ix) Godoro **futi 3-3½,** chandarua moja nyeupe ya pembe nne, mto na foronya nyeupe.
x) Shuka mbili (**02**)rangi ya blue bahari, shuka moja (**01**) jeupe la kutandika siku ya Ijumaa.
xi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
xii) Ndoo mbili (**02**) ndogo zenye mifuniko.
xiii) Kwanja **01**, Jembe **01**, squizer(mopa) **01**, mifagio 02 ya plastic (hard and soft blooms).
xiv) Kanga/ Kitenge na taulo.
xv) Sare ya Michezo (trucksuite ya rangi ya blue) pamoja na raba ya michezo.

**Njoo na ua la kuotesha kwa kuboresha mazingira(Kama unapotoka yapo)**

**3) Msimamo wa Shule:-**

► Nidhamu ya hali ya juu nyakati zote – Exemplary Discipline
► Taaluma kiwango cha juu – Academic Excellence
► Usafi wa hali ya juu – High standard of smartness
► Uongeaji wa lugha ya kiingereza nyakati zote – English speaking

**4) Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:-**

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
iii) Kugoma/ kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**5) Viambatanisho na fomu muhimu.**

a) **Fomu ya Uchunguzi wa Afya** (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) **Fomu ya maelezo binafsi** kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) **Fomu ya mzazi** kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) **Picha nne** za Wazazi 2 na Ndugu wa karibu 2 wa mwanafunzi wanaoweza kuwa msaada kwa mwanafunzi pale ambapo wazazi hawapatikani. Mwanafunzi aje shuleni pamoja na namba zao za simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo yote na kuyatekeleza kikamilifu.**
**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWENDAKULIMA**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……**
**Jina la Mkuu wa Shule ……**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……**

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

**To be completed by a Government Medical Officer in respect of:-**

Pupil's full name: ……..

Blood count (Red and White): ……

Stool Examination: …….

Analysis: …….

Syphilis Test: ……..

Eye Test: …….

Ears: ……

Chest: ……..

Spleen: ……

Abdomen: ……

Pregnance test (for girls)UPT…….

ADDITIONAL INFORMATION: E.g Physical defects or imp nb airments infections, chronic or family disease that needs special attention (if any)

……

I certify that the above is fit/ unfit for admission into a boarding secondary school

Signature: ……

Designation: ……

Station: ……...

Date: ……..

**MAELEZO BAYANA (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)**

1. Jina kamili la mwanafunzi: …….
2. Tarehe ya kuzaliwa: …….
3. Jina la baba/ mlezi: ……...
4. Jina la mama: ……..
5. Kazi afanyayo baba: ……
6. Kazi afanyayo mama: ……..
7. Anuani ya baba/ mama: ……..
8. Mwanafunzi ana kilema chochote? ……
9.Anapendelea kushiriki michezo gani? ……

10. Taja ndugu wanne (**4**) wa karibu wanaoweza kutoa msaada wakati mzazi anapokosekana muda mwanafunzi awapo shuleni. Picha zao (passport size) ziambatanishwe.

| S/N | JINA LA MZAZI/ NDUGU | KAZI AFANYAYO | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|
| **1.** | | | |
| **2.** | | | |
| **3.** | | | |
| **4.** | | | |

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA ULIPAJI WA ADA**

**SEHEMU A: MWANAFUNZI**

Mimi …… ninakiri kuzisoma sheria, kanuni, na taratibu zote za shule hii na ninakubali kuzitekeleza katika kipindi chote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Mwendakulima. Na endapo nitakwenda kinyume cha taratibu zilizopo, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwemo kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Sahihi (isiyo ya kukoroga): ……simu ya baba……

Simu ya mama……..Tarehe: ……

NB: ***Endapo mwanafunzi ataonekana dhaifu katika tahasusi aliyochaguliwa, atashauriwa kubadili tahasusi kulingana na ufaulu wake kidato cha nne.***

**SEHEMU B: MZAZI/ MLEZI**

Mimi mzazi/ mlezi wa mwanafunzi ……..ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, na taratibu za shule. Pia nikiwa kama mzazi/ mlezi wa mwanafunzi husika; ninakiri kukubali kumlipia ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule bila kusita wala kuicheleweshe.

Jina la mzazi/ mlezi: ……..

Sahihi: ……

Tarehe: ……..

**NB.Muda wote mwanafunzi awapo shuleni, ataruhusiwa kutumia simu ya shule 0754383907 au ya mkuu wa shule,makamu au matroni wa shule kwa mawasiliano na mzazi /mlezi kwa mahitaji yake na si vinginevyo.Ukibainika kukiuka sharti hili ,utakuwa umetenda kosa na hatua zakisheria zitachukuliwa dhidi yako.**

**1. Tai**

**2. Kitambaa cha sketi 1**

**3. Shamba dress**